

**TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA**

# HABARIKA NA TACAIDS

## SERIKALI YATENGA TZS BIL. 277 KUGHARAMIA HUDUMA ZA VVU NA UKIMWI

Toleo Na. 001

*Jarida Mtandao*

# SERIKALI YATENGA TZS BIL. 277 KUGHARAMIA HUDUMA ZA VVU NA UKIMWI



Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za VVU na UKIMWI nchini ambapo Kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF), imepanga kutoa zaidi ya Shilingi Bilioni 277 kwa mwaka kugharamia huduma za VVU na UKIMWI.

Hatua hiyo inalenga kupunguza utegemezi wa wafadhili katika kugharamia afua za VVU na UKIMWI hapa nchini.

Akizungumza mara baada ya kutembelea Maonesho ya Nanenane katika Banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu jijini Dodoma, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania -TACAIDS, Dkt. Samwel Sumba, amebainisha kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuimarisha upatikanaji wa fedha za ndani ili kugharamia mwitikio wa UKIMWI

"Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za VVU na UKIMWI ikiwa ni pamoja na huduma za kinga, matibabu kwa WAVIU na matunzo na kuhakikisha Dawa za Kufubaza Virusi Vya UKIMWI wote. Takribani asilimia 90 ya WAVIU wote nchini wanapata huduma za matibabu na matunzo"

Dkt. Sumba alisisitiza kuwa zaidi ya asilimia 91 ya watu waliogundulika kuwa wanaishi na maambukizi ya VVU, wameunganishwa katika huduma za matibabu ya ARV na matunzo katika vituo vya kutolea huduma vilivyopo nchini.

Kupitia maonesho hayo, TACAIDS imetoa elimu kwa wananchi kuhusu VVU na UKIMWI ili kupunguza unyanyapaa ambao ni kikwazo kikubwa katika mwitikio wa UKIMWI.

Aidha, ameongeza kuwa Unyanyapaa umepungua toka asilimia 28 kwa mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 5 mwaka 2024, lengo ni kutokomeza unyanyapaa ifikapo mwaka 2030.

"Tuendelee kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi, Tujitokeze kupima kwa hiari ili kujua hali zetu (upimaji wa VVU ni bure) na Kwa ambao tuna maambukizi basi tuhakikishe tunatumia ARV bila kutetereka"




# TACAIDS YASHIRIKI MAONESHO YA 49 YA SABASABA

Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imeshiriki katika maonesho ya 49 ya kimataifa ya wafanyabiashara (Sabasaba) na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini, Unyanyapaa na Ubaguzi kwa Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU), Matumizi sahihi ya Kondom na Upimaji wa VVU kwa hiari bila malipo

Maonesho hayo yalifanyika katika viwanja vya Sabasaba Jijini Dar Es Salaam na kuhusisha taasisi za Umma na Binafsi ikiwemo TACAIDS kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (NACO-

mchango wa Serikali katika kufanikisha malengo ya kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030.

Maonesho hayo yalitembelewa na Wananchi na Viongozi ambapo katika Banda la TACAIDS huduma za upimaji wa hiari wa VVU na ushauri nasaha ilitolewa na jumla ya watu 209 walipatiwa huduma hiyo wakiwemo wanaume 80 na wanawake 129 , miongoni mwao watu wa 4 walibainika kuwa wanaishi na maambukizi ya VVU na kuunganishwa na huduma za matibabu na matunzo.







# WAZIRI MKUU AIPONGEZA TACAIDS KWA KUIMARISHA URATIBU WA AFUA ZA VVU NA UKIMWI NCHINI.

Kufuatia Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kufanikiwa kuimarisha Udhibiti wa UKIMWI nchini kwa kupunguza maambukizi mapya ya Virusi Vya UKIMWI (VVU), vifo vitokanavyo na UKIMWI pamoja na Unyanyapaa na Ubaguzi kwa Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU).

Hatua hizo zilimsukuma Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa kutoa pongezi kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kutoa elimu ya VVU na UKIMWI, huduma za upimaji

ho ya Nanenane Kitaifa yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma.

Mhe. Majaliwa alitoa pongezi hizo wakati alipotembelea banda la TACAIDS lilokua ndani ya banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Waziri Mkuu alionesha kuridhishwa na namna TACAIDS inavyotoa elimu kuhusu

Pamoja na pongezi hizo alisisitiza iendelee kuratibu utoaji elimu na huduma ya upimaji wa wa VVU kwa hiari kwenye maonesho hayo.



## MATUKIO KATIKA PICHA





Picha za matukio ya wafanyakazi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - TACAIDS wakitoa elimu kwa Viongozi na wananchi kwenye Banda la pamoja la Ofisi ya Waziri Mkuu wakati wa Maonesho ya wakulima Nane nane yaliyofanyika **kitaifa jijini Dodoma.**




# TACAIDS YASHIRIKI KAMPENI YA KILI CHALLENGE

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS kwa kushirikiana na kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) na wadau wengine imetekeleza kampeni ya Kilimanjaro Challenge Against HIV and AIDS- Kili Challenge inayolenga kuchangia jitihada za Serikali katika kutokomeza maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

TACAIDS na kampuni ya GGML kwa kushirikiana na wadau wengine kila mwaka hutekeleza kampeni ya Kili Challenge kwa kupanda kwa miguu na kuzunguka kwa baiskeli mlima Kilimanjaro ambapo hafla ya kuwaaga wapanda mlima na wazunguka mlima kwa baiskeli, ilifanyika Machame gate na hafla ya kuwapokea ilifanyika

Kwa mwaka 2025 jumla ya watu 64 walishiriki kwenye kampeni hii ambapo watu 47 walipanda mlima umbali wa mita 5,895 kutoka usawa wa Bahari kwa miguu na wengine 17 walizunguka mlima kwa baiskeli zaidi ya kilomita 480, Kampeni ya mwaka huu ilifanikiwa kukusanya takribani Dola za Kimarekani 119,750 na Shilingi za Kitanzania milioni 34.3.


Kupitia kampeni hii elimu kwa wananchi kuhusu Mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini, Unyanyapaa na Ubaguzi kwa Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU), Matumizi sahihi ya Kondom na Upimaji wa VVU kwa hiari bila malipo vilitolewa kwenye geti la Machame na Mwika mkoani Kilimanjaro .











# TANZANIA KUWEKA MKAKATI MADHUBUTI KUKABILI VVU NA UKIMWI KWA USHIRIKIANO WA KIKANDA

Tanzania imechukua hatua muhimu katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kushirikiana na mashirika, Taasisi pamoja na sekta mbalimbali kujadili Mkakati wa utekelezaji wa Huduma za kinga.




Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na shirika la umoja wa mataifa linaloshughulikia masuala ya UKIMWI (UNAIDS) pamoja na shirika la maendeleo la umoja wa mataifa (UNDP) wamejadili Mkakati wa Huduma za kinga dhidi ya VVU na UKIMWI wa Mwaka 2024 - 2030 wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).



Kikao Kazi hicho kilifunguliwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Dkt. Samwel Sumba Septemba 18, 2025 jijini Dar es Salaam.



# KAMATI YA PROGRAMU YA REDIO YA ONGEA YAANZA MAANDALIZI YA MSIMU WA TATU

Kamati tendaji ya kitaalamu kutoka Wizara za Kisekta, Wadau wa Maendeleo, Taasisi zisizo za Serikali pamoja na Wadau wa Redio wamekutana jijini Dodoma kuanza

tatu wa programu ya redio ya ONGEA

Programu hiyo inalenga kutoa elimu na burudani kwa vijana ili waweze kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, Mimba katika umri mdogo, Ndoa za utotoni, Afya ya akili, hedhi salama na kuwajengea uwezo wa kujitambua ili waweze kufikia malengo yao

Programu hiyo ambayo imeshafanyika kwa misimu miwili mfululizo imekua ikisaidia jamii kwa kuleta matokeo chanya ya uelewa na elimu juu ya mwitikio wa UKIMWI nchini hususan kwa wanawake na vijana ikiwa ni moja ya mikakati ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania TACAIDS katika harakati za kupambana na maambukizi mapya







# RC KIHONGOSI AIPONGEZA TACAIDS KWA MIKAKATI YA KUDHIBITI UKIMWI NCHINI





Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. Kenani Kihongosi ameipongeza Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania -TACAIDS kwa kufanikiwa kuratibu mikakati ya kudhibiti UKIMWI nchini ambapo kwa mujibu wa

ya mwaka 2022/23 imeainisha kupungua kwa maambukizi mapya ya VVU, vifo vitokanavyo na UKIMWI, unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU).

Mhe. Kihongosi alifafanua kuwa mafanikio hayo ni kufuatia jitihada zinazofanywa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwekeza katika miundo mbinu ya Afya na kuboresha huduma za Afya ikiwemo huduma za VVU na UKIMWI.

Akiongea wakati wa kikao kazi cha Menejimenti na watumishi wa TACAIDS jijini Arusha, Mhe. Kihongosi alifafanua kuwa TACAIDS imekuwa mstari wa mbele katika kuratibu mikakati ya kudhibiti VVU na UKIMWI na kusimamia miradi ya kuzuia maambukizi mapya, kutoa huduma za tiba na matunzo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma sahihi za VVU na UKIMWI

Awali, akizungumza katika kikao hicho, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania -TACAIDS, Dkt. Samwel Sumba, alibainisha kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuimarisha upatikanaji wa fedha za ndani ili kugharamia mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini.

Dkt. Sumba alifafanua kuwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) Serikali imepanga kutoa zaidi ya Bilioni 277 kwa mwaka kugharamia huduma za VVU na UKIMWI kwa lengo la kupunguza utegemezi wa wafadhili katika kugharamia afua za VVU na UKIMWI hapa nchini.

Katika hatua nyingine Dkt. Sumba aliwataka watumishi wa TACAIDS kila mmoja kuwa sehemu ya ushindi katika kudhibiti VVU na UKIMWI, kwa kuwa wabunifu na kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya Tume hiyo ili kuweza kuongeza kasi ya mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini.

# MATUKIO KATIKA PICHA



**Wakuu wa Idara na Vitengo wakitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TACAIDS kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 wakati wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TACAIDS, uliofanyika Agosti 2025, jijini Arusha.**



**Viongozi na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania -TACAIDS, wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa TACAIDS, uliofanyika mwezi Agosti 2025, jijini Arusha.**

# KAMATI MPYA YA UKAGUZI TACAIDS YAPIGWA MSASA WA KUIMARISHA USIMAMIZI NA UTAWALA BORA



Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) ilitoa mafunzo maalum kwa Kamati mpya ya Ukaguzi ya Taasisi hiyo ikiwa ni hatua muhimu ya kuimarisha usimamizi, uwajibikaji na utawala bora ndani ya taasisi.

Mafunzo hayo yalitolewa jijini Dar es Salaam na kufunguliwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dkt. Samwel Sumba, ambaye alitoa msisitizo kwa kamati kuhakikisha inayatambua

kazi kwa ushirikiano wa karibu na menejimenti.

Dkt Sumba alisema"Tunatambua kuwa mafanikio ya taasisi yoyote yanategemea uwazi na uwajibikaji. Mafunzo haya ni jukwaa la kujenga uelewa wa pamoja na kuimarisha misingi ya utawala

Aidha, aliongeza kuwa mafunzo hayo yanatarajiwa kusaidia Kamati ya Ukaguzi kutekeleza

majukumu yake kwa ufanisi zaidi, hususan katika kuhakikisha uadilifu na uwazi kuwa endelevu kwa kila ngazi ya utendaji wa TACAIDS.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ya TACAIDS, David Alal ameishukuru menejimenti ya tume hiyo kwa kuandaa mafunzo hayo, akieleza kuwa yamewasaidia kuelewa kwa kina namna taasisi inavyofanya kazi

"Mafunzo haya yametupa mwanga mpana kuhusu majukumu yetu na jinsi ya kushirikiana na menejimenti kwa ufanisi zaidi,"

Miongoni mwa mada zilizojadiliwa katika mafunzo, ni pamoja na Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Muundo na majukumu ya tume, Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (2021/22 - 2025/26), pamoja na Mpango Mkakati wa TACAIDS wa miaka mitano (2021/22 - 2025/26).

Hatua hii inaonesha dhamira ya TACAIDS kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na kuhakikisha kuwa taasisi inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi, uwazi na kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.











# TACAIDS YAWAPA POLISI MAFUNZO YA KINGA DHIDI YA VVU



Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), kwa ushirikiano na Wizara ya Afya na mashirika ya kimataifa, iliendesha mafunzo ya kinga dhidi ya VVU kwa askari wa Jeshi la Polisi , jijini Dar es Salaam ambao ni wakuu wa vituo ngazi ya wilaya na kata ili waweze kutoa huduma salama kwa jamii.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Idara ya mwitiko wa kitaifa -TACAIDS, Bi. Audrey Njelekela alisema kuwa mafunzo hayo ni hatua ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kutokomeza maambukizi mapya ya VVU nchini.

Amesisitiza kuwa TACAIDS inatambua mchango mkubwa wa vyombo vya ulinzi na usalama katika kufanikisha huduma za afya.

Aidha alisisitiza Mafunzo hayo ni sehemu ya mpango wa kitaifa wa kuhakikisha kila sekta inashiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.

“Jukumu la kutokomeza UKIMWI si la sekta moja pekee, bali ni la kila mmoja wetu kuanzia familia, jamii, taasisi za serikali hadi vyombo vya ulinzi"Alisema Bi Audrey Njelekela

Kwa upande wake, Kamishna wa Polisi wa Jamii, Faustine Shilogile akifunga mafunzo hayo, ameishukuru TACAIDS na wadau wote waliofanikisha zoezi hilo ambapo amebainisha kuwa watayatumia maarifa hayo katika utekelezaji wa majukumu yao hasa watapokuwa wakihudumia wananchi wanaohitaji msaada wa haraka na wa kiutu.

"Mafunzo hayo yalijikita katika elimu mahususi ya Matumizi sahihi ya kondomu ya Kike na kiume, Magonjwa ya ngono, Elimu ya kujipima VVU.

Masuala mengine ni Umuhimu na matumizi ya ARV, Matumizi ya dawa ya kuzuia maambukizi ya VVU baada ya hatari ya maambukizi ya VVU (PEP) na matumizi ya dawa ya kuzuia maambukizi ya VVU kabla ya hatari ya maabukizi ya VVU (PrEP)

TUME YA KUDHIBITI UKIMWI
TANZANIA
COMMISSION FOR AIDS
TACAIDS

@tacaidsinfo

@tacaidsinfo

@tacaidsinfo

@tacaidsinfo

**Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**
S.L.P 2904
Nanenane, Nzuguni
DODOMA
Barua pepe:
info@tacaids.go.tz
Tovuti:
www.tacaids.go.tz